**MKATABA WA HUDUMA YA UFUNDI WA UKARABATI WA JENGO LA UANGALIZI MAALUM (ICU) KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SONGEA**

**KATI YA**

**MGANGA MFAWIDHI**
**(MWAJIRI)**

**NA**

**FRANSISCO MAPUNDA**
**(MWAJIRIWA)**

# FOMU YA MAKUBALIANO YA MKATABA

Makubaliano haya ya Mkataba yanafanywa leo..03... siku ya ..01/2022.., Kati ya **MGANGA MFAWIDHI – HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SONGEA, S.L.P 05 SONGEA** (Hapa ataitwa "Mwajiri") kwa upande mmoja

**NA**

**FRANSISCO MAPUNDA** mwenye namba za simu **0762105820** (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Fundi Kiongozi) kwa upande mwingine.

**KWA KUWA** Mwajiri anahitaji na yuko tayari kumwajiri Fundi kiongozi kwa ajili ya kutoa Huduma ya ufundi wa ukarabati wa jengo la uangalizi maalum (ICU) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea kupitia **Mkataba Na. ME/007/2021/2022/SORRH/W/02** wenye jumla ya **Tshs 29,820,000** Hapa itaitwa ("Bei ya Mkataba").

**SASA MAKUBALIANO HAYA YAMESHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO:**

1. **KWAMBA** katika makubaliano haya maneno na maelezo yatakuwa na maana sawa kama yalivyopewa katika Masharti ya Mkataba unaolejelewa.

2. **KWAMBA** nyaraka zifuatazo zitachukuliwa kwa pamoja na zisomeke na kufasiriwa kuwa ni sehemu ya makubaliano haya, yaani;

    i) Fomu ya Makubaliano ya Mkataba;
    ii) Barua ya Kukubali Kotesheni;
    iii) Fomu ya Kuwasilisha Kotesheni;
    iv) Masharti Maalumu ya Mkataba;
    v) Masharti ya Jumla ya Mkataba;
    vi) Uainishaji Viwango na Vipimo Kiufundi, kama upo;
    viii) Michoro,
    viii) Maelezo ya Mahitaji na Orodha ya Bei;
    ix) Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba (Kumbukumbu za ufafanuzi, memoranda dhidi ya rushwa).

3. **KWAMBA** nyaraka zote zilizotajwa hapo juu zitarejelewa hapo baadaye kama 'Mkataba' na zitachukuliwa kuwa zinakamilishana na zinajieleza sawa lakini ukitokea utata au uhitilafiano zitakuwa na umuhimu katika mfuatano wake kama zinavyoonyeshwa hapo juu.

4. **KWAMBA** katika kuzingatia malipo yanayofanywa na Mwajiri kwa **Fundi kiongozi** kama baadaye inavyotajwa, **Fundi kiongozi** hapa anakubaliana na Mwajiri kutekeleza na kukamilisha Huduma ya ukarabati kwa kufuata makubaliano, kwa hali zote zile na kulingana na vifungu vya mkataba.

5. **KWAMBA** Mwajiri anakubali kumlipa Fundi kiongozi kwa kuzingatia utekelezaji na ukamilishaji wa Utoaji huduma, jumla ya Shilingi za Kitanzania **Milioni ishirini na Tisa mia nane na ishirini elfu tu Tshs 29,820,000** baadaye imerejelewa kama "Bei ya Mkataba" kwa nyakati na namna iliyoelezwa katika mkataba.

6. **KWAMBA** Mwajiri atakata kodi ya zuio ya asilimia tano (5%) kwenye kila malipo ya Fundi kiongozi yanapofanyika

7. **KWAMBA** Mkataba huu ni wa muda wa mwezi mmoja kuanzia tarehe 05/01/2022 mpaka tarehe 04/02/2022

8. **KWAMBA** Mwajiri atakuwa na wajibu wa kutoa vifaa vya Ujenzi vya kiwandani na visivyo vya kiwandani vitakavyoainishwa na Mhandisi wa Ujenzi kwa ajili ya kazi ya ukarabati.

9. **KWAMBA** Mwajiri atakuwa na wajibu wa kutunza vifaa vilivyonunuliwa.

10. **KWAMBA** Malipo ya kipengele namba tano (05) yatafanywa kulingana na kazi iliyofanyika na kithibitishwa na Mhandisi wa Ujenzi.

11. **KWAMBA** Hakutakuwa na mabadiliko ya aina yoyote katika kipindi chote cha Mkataba.

12. **KWAMBA** Fundi kiongozi anapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia michoro na maelekezo ya kitaalamu kutoka kwa Mhandisi wa Ujenzi.

13. **KWAMBA** Fundi kiongozi anatakiwa kutunza siri za Mwajiri atakazo zijua katika kipindi chote cha Mkataba huu.

14. **KWAMBA** Fundi kiongozi anatakiwa kuhakikisha kuwa eneo la Ujenzi ni safi muda wote.

15. **KWAMBA** Fundi kiongozi atakuwa na wajibu wa kufanya kazi kwa uaminifu na pasipo kumsababishia hasara yoyote mwajiri

16. **KWAMBA** Fundi kiongozi anatakiwa kutumia sehemu ya malipo yake kwa ajili ya kuwalipa wasaidizi wake wa kazi na kutosababisha mgogoro wowote wa malipo katika eneo la Ujenzi.

17. **KWAMBA** Mwajiri atakuwa na haki ya kuvunja Mkataba huu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Fundi kiongozi pale Fundi kiongozi atakapokuwa amekiuka Mkataba huu, akielezea nia yake ya kuvunja Mkataba ndani ya siku saba (07).

18. **KWAMBA** Fundi kiongozi atakuwa na haki ya kuvunja Mkataba huu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Mwajiri pale Mwajiri atakapokuwa amekiuka Mkataba huu, akielezea nia yake ya kuvunja Mkataba ndani ya siku saba (07).

19. **KWAMBA** Endapo kutakuwa na hasara yoyote iliyosababishwa na Fundi kiongozi, Fundi kiongozi atakuwa na wajibu wa kulipa gharama za hasara alizozisababisha au kukatwa malipo yake ili kufidia hasara iliyosababishwa.

20. **KWAMBA** Endapo kama kutakuwa na ucheleweshwaji wa kazi uliosababishwa na mwajiri, mwajiri atamwongeza muda wa kazi Fundi kiongozi.

21. **KWAMBA** Mwajiri atatoa kusudio la kuvunja Mkataba kwa maandishi ndani ya siku saba (07).

22. **KWAMBA** Endapo kutatokea mgogoro baina ya pande zote mbili basi mgogoro huo utatatuliwa kwa njia ya mazungumzo kwanza na maafikiano yatakuwa sehemu ya mkataba. Migogoro hiyo ikishindwa kutatulika kwa njia ya mazungumzo basi hatua za kisheria zitachukuliwa na upande utakaoona inafaa kufanya hivyo, endapo kutatokea mgogoro wowote.

23. **KWAMBA** Hakutakuwa na mabadiliko yoyote katika Mkataba huu bila pande zote mbili za mkataba huu kukubaliana na endapo kutokea mabadiliko basi mabadiliko hayo yatapata ridhaa ya maandishi kutoka kwa Mwajiri na mabadiliko hayo yatatengenezwa kama nyongeza katika Mkataba huu.

24. **KWAMBA** Haki za kimkataba hazitaathirika baada ya mkataba kuvunjika.

25. **KWAMBA** mkataba huu ni halali kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utatafsiriwa kwa mujibu wa sheria hizi

**KATIKA KUSHUHUDIA**, pande hizi zimefanya makubaliano ya kutekelezwa kulingana na sheria katika siku na mwaka kama ulivyoandikwa hapo juu.

**IMETIWA SAINI KWA AJILI YA**
**NA KWA NIABA YA MWAJIRI**

**YAMESAINIWA** na **KUTOLEWA** na

Saini:..............................

Jina: ...........DR MAGARU MAJURA...........

MEDICAL OFFICER INCHARGE
SONGEA REGIONAL REFERRAL HOSPITAL
P. O. Box 5, SONGEA

Cheo: **MGANGA MFAWIDHI**

Tarehe 03 ....Mwezi 01 ....2022

Saini.................................

Jina: Franc Hoza ..................................................

Cheo**: MHANDISI WA UJENZI**

Tarehe..........Mwezi.........2022

**YAMESAININIWA** na **KUTOLEWA** na

Saini ........................................................

Jina**:** FRANCISCO G. MAPUNDA

Cheo**: FUNDI KIONGOZI**

Tarehe.. 03 ...Mwezi.. 01 ...2022

Saini:.. 03 ........ 01 .........................

Jina: RAJABU RAJABU ndomba

**Cheo: SHAHIDI WA FUNDI KIONGOZI**

Tarehe.. 03 .....Mwezi.. 01 ....2022

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO.**

**MKOA WA RUVUMA**

Anwani AFYA
Simu Na. 025-2602048
Fax Na. 025-2602048
**E-mail :songearrh@afya.go.tz**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa
S.L.P. 5,
**SONGEA**

Kumb.Na.AFY/B.2/VOL.IX/3

02/12/2021

Fransisco Mapunda,
**FUNDI KIONGOZI,**
Simu Na. 0762105820,
**SONGEA**

**YAH: BARUA YA KUKUBALI KOTESHENI**

Tafadhali husika na kichwa cha Habari hapo juu.

2. Hii ni kukutaarifu kuwa kotesheni yako ya tarehe 23/11/2021 ya kutoa Huduma ya ukarabati wa jengo la uangalizi maalum (ICU) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Songea, Kotesheni Na. **ME/007/2021/2022/SORRH/W/02** kwa bei ya Mkataba ya **Shilingi za Kitanzania milioni ishirini na tisa mia nane na ishirini elfu (TZS 29,820,000)** utakaotekelezwa kwa muda wa siku thelathini **(Siku 30)** kama ilivyosahihishwa na kurekebishwa ipasavyo na maelekezo kwa Fundi Kiongozi (Mwajiriwa) sasa imekubaliwa.

3. Unatakiwa kuja hapa ofisini tarehe 03/12/2021 kuweka saini Makubaliano ya Mkataba na kuanza kutoa huduma katika muda uliokubaliwa kutoka siku mkataba utakapotiwa saini.

4. Nakutakia utekelezaji mwema.

Dr. Magafu Majura
**MGANGA MFAWIDHI**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SONGEA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SEREKEALI ZA MITAA**

MKOA WA RUVUMA
Simu Nambari. *025-2602256/2602238*
Fax No. 2602144
E-mail: ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
Tovuti: www.ruvuma.go.tz

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L. P. 74,
**SONGEA.**

# FOMU YA KUWASILISHA KOTESHENI

23/11/2021 *[Tarehe]*

Kwa: [FRANCISCO GABRIEL MAPUNDA

Tunaahidi kutoa HUDUMA YA UFUNDI WA UKARABATI LA JENGO UANGALIZI MAALUMU (ICU) KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SONGEA- ME/007/2021/2022/SORRH/W/02 *[Ingiza maelezo ya huduma na namba ya Kotesheni ]* kulingana na Masharti ya Mkataba yanayofuatana na Kotesheni hii kwa bei ya Mkataba ya TSH. 29,820,000 MILIONI ISHIRINI NA TISA LAKI NANE NA ISHIRINI ELFU TU.

*[Ingiza kiasi katika maneno, tarakimu na aina ya sarafu]*

Pia tunaahidi kukamilisha huduma iliyotajwa katika kipindi cha MWEZI MMOJA *[Ingiza kipindi]* ambacho kinajumuisha kipindi cha maandalizi.

Kotesheni hii pamoja na barua yako ya kukubali kwa maandishi vitafanya mkataba unaotufunga sisi pamoja. Tunafahamu kuwa hulazimiki kukubali kiwango cha chini au kotesheni yoyote kati ya kotesheni unazopokea.

Tunathibitisha kuwa kotesheni hii imetimiza masharti kama yanavyotajwa katika Mwaliko wa Kotesheni.

Jina la Mwombaji (Fundi) FRANCISCO GABIEL MAPUNDA

Akaunti namba ya benki 01J2093857700

Jina la benki malipo yatakapofanyika CRDB

Mahali mwombaji anapopatikana..........mtaa/barabara/kitongoji MKUZO

Anwani ya Posta PO BOX 3032 Simu/Fax 0762 105 820

Sahihi [signature] Tarehe 23 mwezi 11 mwaka 2021

# SEHEMU V: MASHARTI MAALUMU YA MKATABA

Taarifa maalumu ifuatayo kwa ajili ya Huduma Zisizo za Ushauri wa Kitaalamu zinazonunuliwa na itakuwa nyongeza, au inaweza kurekebisha vifungu katika **Masharti ya Jumla ya Mkataba**. Kunapokuwa na mgogoro, vifungu katika Masharti Maalumu ya Mkataba vitakuwa na nguvu zaidi ya vifungu katika **Masharti ya Jumla ya Mkataba.**

| Masharti Maalumu ya Mkataba Kifungu Na. | Masharti ya Jumla ya Mkataba Kifungu Na. | Marekebisho ya, na Nyongeza kwa vifungu katika Masharti ya Jumla ya Mkataba |
|---|---|---|
| 1 | 4.0 | Lugha ya Mkataba: *[KISWAHILI]* |
| 2 | 19.0 | Mkataba Unaanza tarehe: [*MARA TU* ] baada ya siku ya kutia sahihi mkataba. |
| 3 | 19.0 | Muda wa kukamilisha [MIEZI MIWILI] kutoka tarehe ya kuanza mkataba. |
| 4 | 21.1 | Malipo ya awali (kama yatalipwa) ni *[***HAKUNA MALIPO YA AWALI**]. |
| 5 | 21.2 | Asilimia ya fedha za kushikiliwa: [*100%*] ya thamani ya madai kwa mwezi huo. HAKUNA<br><br>Fedha iliyoshikiliwa itatolewa katika [*Ndani ya siku saba*] baada ya kukamilika kwa mkataba. HAKUNA<br><br>Fedha kwa ajili ya kodi ya zuio: Mtoa Huduma atakatwa asilimia tano (5%) katika kila malipo yake ikiwa ni fedha kwa ajili ya kodi ya zuio kwa Serikali.<br><br>Kiasi anachopaswa kulipwa **Mtoa Huduma** chini ya Ankara yoyote kitalipwa na Mteja kwa **Mtoa Huduma** katika [*ndani ya siku saba*] baada ya **Mtoa Huduma** kuwasilisha Ankara. HAKUNA |
| 6 | 21.4 | Kama Mteja atashindwa kufanya malipo katika [*muda wa siku saba baada ya kazi kukamilika*] Mteja atamlipa **Mtoa Huduma** riba katika kima [*0.1% ya mkataba kila siku kwa siku zitakazoongezeka*] HAKUNA |
| 7 | 23.2 | Mwamuzi atakuwa [*MWANASHERIA WA SERIKALI*] |
| 8 | 23.3 | Kima cha ada ya Mwamuzi kitakuwa [*ITAKUBALIKA*]<br><br>Aina ya gharama zitakazorudishwa zitakuwa[*HAKUNA* ] |
| 9 | 23.4 | Mamlaka ya kuteua Mwamuzi ni [*ITAKUBALIKA*] |
| 10 | 23.6 | Taasisi ya Usuluhishi itakuwa [*ITAKUBALIKA*]<br><br>Mahali pa kufanyia Usuluhishi [*SONGEA*] |

# SEHEMU IV: MASHARTI YA JUMLA YA MKATABA

## A: VIFUNGU VYA JUMLA

### Kifungu 1: Nyaraka za Mkataba

Masharti ya Mkataba na fomu ya Malezo ya mahitaji, Viwango na Vipimo ni sehemu muhimu ya nyaraka za Mkataba na zinapaswa kusomwa pamoja na nyaraka nyingine zote zinazounda Mkataba. Kama ikitokea kuna mgogoro, kipaumbele cha nyaraka kitakuwa kama ilivyoainishwa katika **Kifungu cha 6** cha Masharti haya ya Mkataba.

### Kifungu 2: Tafsiri

Katika Masharti haya ya Mkataba maneno yafuatayo yatakuwa na maana zilizotolewa kwayo kama ilivyo hapa chini:

| | |
|---|---|
| **Mteja** | Taasisi ya Serikali inayonunua huduma kama zilivyotajwa kwenye mkataba. |
| **Mtoa Huduma** | Mtu au watu au kampuni ambayo kotesheni yao imekubaliwa na mteja. |
| **Huduma** | Huduma itakayotolewa kulingana na mkataba. |

### Kifungu 3: Maelekezo

Maelekezo yanayotolewa na Mteja yatakuwa kwa maandishi. Kwa sababu nyingine yoyote ile maelekezo hayo yakatolewa kwa mdomo, Mtoa Huduma atafuata maelekezo hayo. Katika kipindi cha **siku 7** maelekezo yaliyotolewa kwa mdomo yanapaswa kuwa yamethibitishwa kwa maandishi.

### Kifungu 4: Lugha

Matangazo yote, maelekezo na mawasiliano au waraka wowote wa maandishi unaohusu mkataba utaelezwa bayana katika Masharti Maalumu ya Mkataba.

### Kifungu 5: Sheria inayotumika

Mkataba, maana yake, fasiri yake, na utekelezaji wake vitaongozwa na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Kifungu 6: Nyaraka za Mkataba zenye Kipaumbele**

Nyaraka kadhaa zinazofanya mkataba zichukuliwe kuwa zinajieleza kikamilifu lakini kama ikitokea hitilafu yoyote ile nyaraka zenye umuhimu wa kwanza zitakuwa zifuatazo:

i) Fomu ya Makubaliano;
ii) Barua ya Kukubali Kotesheni;
iii) Fomu ya Kuwasilisha Kotesheni;
iv) Masharti Maalumu ya Mkataba;
v) Masharti ya Jumla ya Mkataba;
vi) Maelezo ya Mahitaji na Orodha ya Bei; na
vii) Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba huu (Kumbukumbu za ufafanuzi, memoranda dhidi ya rushwa).

**B: MAJUKUMU**

**Kifungu 7: Utekelezaji wa Mkataba**

**Mtoa Huduma** atatoa nguvu kazi yote, zana, usafiri, maunzi na cho chote kile kinachohitajika katika utoaji wa huduma. **Mtoa huduma** atatoa huduma kulingana na inavyotakiwa na nyaraka za mkataba, na maelekezo ya ziada kama yatakavyotolewa mara kwa mara.

**Kifungu 8: Kutoa kazi kwa Mtoa Huduma Msaidizi**

**Mtoa Huduma** hatatoa kazi au sehemu ya kazi kwa Mtoa Huduma saidizi bila kibali cha maandishi cha kutoka kwa Mteja. Kibali kama hicho kinapotolewa hakimwondolei **Mtoa huduma** mamlaka au majukumu yake chini ya mkataba na **Mtoa huduma** atakuwa na wajibu kwa kushindwa au kuzembea kwa yeyote kati ya watoa huduma wake wasaidizi.

**Kifungu 9: Usimamizi wa Kazi wa Mtoa Huduma**

**Mtoa Huduma** atatoa huduma kwa uangalifu na kwa kufuata utendaji unaotakiwa na Mteja ili kufikia mahitaji maalumu ya ubora, wingi na muda uliopangwa. Kama katika wakati wowote ule Mteja anaona uzembe, au kubadilika sana kwa mwelekeo kutoka katika kawaida zilizowekwa, hatua zinazofaa zitachukuliwa na **Mtoa Huduma** ili kurekebisha hali.

**Kifungu 10: Ukaguzi**

Mteja au mwakilishi wake aliyempa mamlaka ana haki ya kukagua huduma na **Mtoa Huduma** atatoa ushirikiano unaofaa wakati Mteja atakapohitaji kufanya hiyo.

**Kifungu 11: Huduma Zilizokataliwa**

Huduma zisizofuata mahitaji ya mkataba zitakataliwa. Kwa maelekezo ya Mteja, Mtoa huduma kwa gharama zake mwenyewe atarekebisha au kutoa upya huduma itakayokuwa imekataliwa hadi kumridhisha Mteja kikamilifu.

**Kifungu 12: Bima**

**Mtoa Huduma** ataweka bima yenye jina lake na la Mwajiri kwa ajili ya hasara au uharibifu wa zana, mitambo na maunzi, wizi na hali nyingine zinazolingana na hizo kwenye Ofisi ya Mwajiri, ambayo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa wafanyakazi wa Mtoa huduma. Mtoa huduma pia atatoa bima kwa ufidiaji majeruhi binafsi au kifo cha mfanyakazi wa **Mtoa Huduma** awapo kazini.

**Kifungu 13: Wajibu wa Mtoa Huduma**

**Mtoa Huduma** atamkinga Mwajiri dhidi ya hasara au uharibifu wa upande wa tatu. Atamkinga kikamilifu Mwajiri wake dhidi ya madeni na hasara zinazotokana na Sheria ya Ajira na Fidia ya Wafanyakazi.

**Kifungu 14: Jambo Lisilozuilika**

Katika tukio la hasara yoyote au uharibifu unaotokea katika utendaji wa aina yoyote wa nguvu za asili ambao pande zote za mkataba kwa hali ya kawaida zisingeweza kutabiri mapema, hasara au uharibifu kama huo utagharimiwa na **Mwajiri** na **Mtoa Huduma**

**Kifungu 15: Ubora wa Huduma na Usanifu wa Kazi**

Huduma zote na usanifu wa kazi vitakuwa vya aina na ubora kama ilivyofafanuliwa katika Mkataba na kulingana na maelekezo ya Mteja na vitaingizwa katika vipimo kama Mteja atakavyotaka.

**Kifungu 16: Upatikanaji wa Maunzi**

**Mtoa Huduma** atabainisha vyanzo vyote vya maunzi yanayohitajika kabla ya kuanza kutoa huduma. Mwajiri atalazimika kama itahitajika upatikanaji wa vyanzo vya maunzi hayo. **Mtoa Huduma** hatatumia maunzi yaliyobainiwa bila kuwa na kibali cha maandishi toka kwa Mwajiri.

**Kifungu 17: Kuondoka Eneo la Kutolea Huduma**

Baada ya kumaliza kutoa huduma, Mtoa huduma ataondoa zana zote, maunzi ya ziada na uchafu katika eneo la kutolea huduma na kuacha eneo hilo likiwa safi na katika hali itakayokubaliwa na Mwajiri.

**Kifungu 18: Afya, Usalama na Kulinda Mazingira.**

**Mtoa huduma** katika kipindi chote cha mkataba atazingatia kikamilifu masuala ya kiafya na kiusalama katika kanda yake ya kazi na watu wote wanaopaswa kuwa katika eneo la kazi katika hali ya mpango mzuri ili kuepusha hatari yoyote kwa watu hao.

**Mtoa Huduma** atazingatia mahitaji na kanuni zote za mazingira kama zinavyoelezwa na Serikali ya Tanzania.

**Kifungu 19: Kuanza na Kukamilika Utoaji Huduma.**

**Mtoa Huduma** ataanza na kukamilisha huduma katika muda uliyoelezwa kwenye Masharti Maalumu ya Mkataba au katika kipindi cha mkataba cha nyongeza, kama kipindi hicho kimeruhusiwa na Mteja.

**Kifungu 20: Ubadilishaji**

Mteja anaweza kubadilisha umbo, ubora au kiasi cha huduma na atakuwa na mamlaka ya kumwagiza **Mtoa Huduma** ipasavyo. Ubadilishaji huo utakuwa kwa Agizo la Mabadiliko ya Mkataba. Mteja ataamua kuhusu kiasi (kama itatokea) ambacho kwa maoni yake kinapaswa kuongezwa au kupunguzwa kutoka jumla ya fedha iliyotajwa kwenye Mkataba kwa ajili ya kazi yoyote ya nyongeza iliyofanywa au iliyoachwa kwa agizo hilo. Kiasi cha fedha kitakachoamuliwa kitatokana na kima cha kizio kwenye Kotesheni au kama hakuna kima cha kizio kinachotumika, kiwango kingine kitatumika kama itakavyoamriwa na Mteja na kukubaliwa na **Mtoa Huduma.**

## C: MALIPO

**Kifungu 21: Malipo**

**21.1 Malipo ya Awali**

Malipo ya awali ya asilimia iliyotajwa kwenye Masharti Maalumu ya Mkataba ya thamani ya mkataba yanaweza

kutolewa baada ya kuwasilisha dhamana inayokubalika katika Masharti Maalumu ya Mkataba. Malipo haya ya awali yatakatwa kwa awamu zinazolingana kwa kila bili itakayowasilishwa na Mtoa Huduma, na lazima zilipwe zote.

### 21.2 Malipo wakati Kazi inaendelea

Malipo yatafanywa kwa **Mtoa Huduma** wakati kazi inaendelea kila mwezi baada ya kuwasilisha ankara kama huduma iliyotolewa inalingana na masharti ya mkataba. Kwa kila ankara kiasi cha fedha kilichotajwa kwenye Masharti Maalum ya Mkataba kitashikiliwa lakini hakitazidi asilimia 10 ya bei ya mkataba. Fedha iliyoshikiliwa itatolewa katika kipindi kitakachokuwa kimeonyeshwa kwenye Masharti Maalumu ya Mkataba

Fedha anayotakiwa kulipwa **Mtoa Huduma** chini ya Ankara yoyote ile italipwa na Mwajiri kwenda kwa Mtoa Huduma katika kipindi kitakachokuwa kimetajwa katika Masharti Maalumu ya Mkataba baada ya Ankara kuwasilishwa na **Mtoa huduma**.

### 21.3 Malipo ya Mwisho

Ankara ya mwisho italipwa katika siku 28 za kazi baada ya tarehe ya kuwasilishwa kwa Mteja ilimradi huduma zote, masahihisho na matengenezo, kama yapo yatakuwa yametekelezwa katika kiwango kitakachomridhisha Mteja.

### 21.4 Ucheleweshwaji wa Malipo

Kama Mteja atashindwa kufanya malipo katika muda uliotajwa, Mteja atamlipa **Mtoa Huduma** riba katika kiwango kilichotajwa kwenye Masharti Maalumu ya Mkataba.

### 21.5 Makato ya Malipo

Mteja atakuwa na haki ya kukata fedha kiasi chochote, fedha ya malipo ya awali au madeni yanayolipika kutoka kwa **Mtoa Huduma** kwenda kwa Mteja kutokana na fedha yoyote anayoweza kulipwa **Mtoa Huduma** na Mteja chini ya mkataba huu ilimradi kifungu hiki hakitaathiri marekebisho yoyote kwa amri ya sheria pengine ambayo mteja anaweza kuwa na haki ya kurudishiwa fedha yoyote kama hiyo.

### 21.6 Malipo kwa Wafanyakazi

Kama kutatokea kushindwa kulipa mishahara/ujira na fidia nyingine zinazopaswa kulipwa wafanyakazi na /au malipo ya kukodisha zana/magari na vifaa chini ya mkataba huu, mteja atakuwa na haki ya kushikilia malipo ya **Mtoa Huduma.** Mteja atatumia fedha alizoshikilia kuwalipa wafanyakazi wa **Mtoa Huduma** mishahara yao na fidia nyingine na madeni ya kukodisha vifaa. Malipo kama hayo yatachukuliwa kuwa ni malipo yaliyopokelewa na **Mtoa Huduma** kutoka kwa Mteja chini ya mkataba huu.

### Kifungu 22: Malipo ya Ucheleweshaji Huduma

Kama Mtoa Huduma atashindwa kutoa huduma katika muda uliotajwa kwenye mkataba au katika muda wowote wa nyongeza ulioruhusiwa na Mwajiri, **Mtoa Huduma** atamlipa Mteja malipo ya ucheleweshaji katika kiwango cha asilimia 0.1 cha thamani ya mkataba kwa siku hadi kiwango cha juu cha asilimia 10 ya bei ya mkataba.

## D: KUSULUHISHA MIGOGORO NA KUVUNJA MKATABA

### Kifungu 23: Kusuluhisha Migogoro

23.1 Kama migogoro ikitokea itasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote. Kama baada ya siku thelathini (30) pande hizo zimeshindwa kumaliza mgogoro au tofauti zao kwa majadiliano ya pamoja, upande wowote ule utawasilisha mgogoro huo kwa maandishi kwa Mwamuzi na kutoa nakala kwa upande mwingine.

23.2 Mwamuzi aliyetajwa katika **Masharti Maalumu ya Mkataba** atatoa maamuzi kwa maandishi katika muda wa siku ishirini na nane (28) baada ya kupokea taarifa ya mgogoro.

23.3 Mwamuzi atalipwa kwa saa kwa kiwango kilichotajwa kwenye **Masharti Maalumu ya Mkataba** pamoja na kurudishiwa gharama za aina ya matumizi kama yalivyobainishwa katika **Masharti Maalumu ya Mkataba** na gharama hiyo itagawanywa kati ya Mteja na **Mtoa Huduma** kwa uamuzi wowote utakaofikiwa na Mwamuzi. Upande wowote unaweza kupeleka uamuzi wa Mwamuzi kwa Msuluhishi kwa maandishi katika

kipindi cha siku ishirini na nane (28) baada ya uamuzi ya Mwamuzi. Kama hakuna upande wowote utakaokuwa umepeleka mgogoro kwa Msuluhishi katika muda wa siku ishirini na nane (28) zilizotajwa hapo juu, uamuzi wa Mwamuzi utakuwa ndiyo wa mwisho na itabidi ufuatwe.

23.4 Kama Mwamuzi atajiuzulu au kufariki au kama Mteja na **Mtoa Huduma** wakikubaliana kuwa Mwamuzi hafanyi kazi yake ipasavyo kulingana na vifungu vya Mkataba, Mwamuzi mpya atateuliwa kwa pamoja kati ya Mteja na **Mtoa Huduma.** Kama kuna kutokubaliana kati ya Mwajiri na **Mtoa Huduma** katika muda wa siku 30, Mwamuzi atateuliwa na Mamlaka ya kuteua itakayotajwa katika **Masharti Maalumu ya Mkataba** kwa maombi ya upande wowote katika muda wa siku kumi na nne (14) tangu kupokelewa kwa ombi hilo.

23.5 Mgogoro au tofauti yoyote ambapo notisi ya kusudio la kuanza usuluhishi imetolewa kulingana na kifungu hiki itamalizwa kwa usuluhishi. Usuluhishi unaweza kuanza kabla au baada ya kuanza kutoa huduma chini ya mkataba.

23.6 Usuluhishi utaendeshwa kulingana na taratibu za usuluhishi kama zilivyochapishwa na taasisi iliyotajwa na mahali palipoonyeshwa katika **Masharti Maalumu ya Mkataba.**

23.7 Bila kujali uwepo kwa usuluhishi wa aina yoyote,

(a) Pande zote zitaendelea kutekeleza majukumu yao chini ya mkataba isipokuwa kama wakikubaliana vinginevyo; na

(b) Mwajiri atamlipa Mtoa Huduma fedha yoyote Mtoa Huduma anayodai.

**Kifungu 24: Uvunjaji wa Mkataba**

24.1 Kama **Mtoa Huduma** anashindwa kuanza kutoa huduma katika muda uliopangwa au kuna sababu za kutosha kuamini kuwa hatakamilisha huduma katika muda uliopangwa au kuna ucheleweshaji uliokiuka tarehe ya kukamilisha au anashindwa kufuata moja ya masharti au hafuati maelekezo ya Mteja au anakuwa mufilisi, Mwajiri

atakuwa na haki ya kuvunja mkataba na kumwajiri **Mtoa Huduma** mpya wa kutoa huduma hiyo.

24.2 Kama Mteja atashindwa kumlipa **Mtoa Huduma** katika muda wa siku 60 baada ya tarehe ya kuwasilisha madai, Mtoa Huduma atakuwa na haki ya kuvunja mkataba.

**Kifungu 25: Malipo kama Mkataba Umevunjwa**

Kama Mkataba umevunjwa, **Mtoa Huduma** atalipwa na Mteja fedha au maunzi yatakayokuwa bado hayajalipiwa katika malipo atakayokuwa amelipwa **Mtoa Huduma** kwa huduma zote zitakazokuwa zimetolewa kabla ya kuvunja mkataba kwa kima na bei kama ilivyotolewa kwenye Mkataba. Ilimradi tu wakati wote itakuwa dhidi ya malipo yoyote yaliyo tayari kutoka kwa Mteja chini ya kifungu hiki, Mwajiri atakuwa na haki ya kulipwa fedha yoyote toka kwa **Mtoa Huduma** iliyotokana na malipo ya awali, kutokana na mitambo/zana/magari na maunzi, na kiasi cho chote alicholipwa **Mtoa Huduma** na Mteja kwa ajili ya utoaji wa huduma.

## SEHEMU VII: MICHORO - HAKUNA

## MAELEZO UKARABATI UTATOLEWA NA MHANDISI WA MRADI

## UKARABATI WA NYUMBA JENGO LA WAGONJWA WANAOHITAJI UANGALIZI MAALUMU (ICU)

| Na | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI |
|---|---|---|
| | | |
| A | **KUBOA** | |
| 1 | Kutindua malumalu zilizopo na kukabidhi vifaa kwa uongozi | 4,000,000= |
| 2 | Kurekebisha mifumo wa maji safi na taka na kukabidhi vifaa | 3,000,000= |
| 3 | Toa milango miwili kadiri ya maelekezo ya msimamizi wa kazi | 30,000= |
| 4 | Toa vitasa vya milango nane na uweke vipya kadiri ya maelekezo ya msimamizi wa kazi | 80,000= |
| 5 | Kurekebisha mivujo yote ya paa na dari | 200,000= |
| 6 | Kutoa dari, mbao na mikanda | 1,200,000= |
| | | |
| B | **KAZI MPYA** | |
| 1 | Kujenga mfereji kwa kutumia tofali | 300000= |
| 2 | Kutandika malumalu | 7,000,000= |
| 3 | Kufyatua mifuniko ya mfareji | 400,000= |
| 4 | Kufitisha grill moja kadiri ya maelekezo | 10,000= |
| 5 | Kutandaza mfumo wa hewa ya Oksijen (Kazi itafanywa na fundi maalumu lakini atalipwa na fundi kiongozi) | 8,500,000= |
| 6 | Kukwangua rangi, kuskimu na kupaka rangi mikono mitatu nje na ndani ya jengo | 1,000,000= |
| 7 | Kutandaza mfumo mpya wa umeme | 300,000= |
| 8 | Kupaka vanishi mikono mitatu katika milango yote ya mbao | 100,000= |
| 9 | Kupaka rangi dari | 500,000= |
| 10 | Kupiga dari | 2,000,000= |
| 11 | Kufunga mikanda ya dari | 200,000= |
| 12 | Kumwaga zege na kutengeneza mfumo wa eneo la kukaushia nguo kwa kutumia jua | 1,000,000= |
| | **JUMLA KUU SHS** | 29,820,000= |
| | | |

**AHADI YA MTOA HUDUMA KUHUSU SERA DHIDI YA RUSHWA, KANUNI ZA MAADILI NA PROGRAMU YA UKUBALIFU**

Sisi/Mimi ....FRANCISCO GABRIEL MAPUNDA.... tunaweka umuhimu katika zabuni ya ushindani unaofanyika kwa misingi ya haki na huru na isiyoruhusu ukiukwaji wa taratibu na kanuni. Tunapenda kuthibitisha kuwa hatutatoa wala kuwezesha moja kwa moja au siyo moja kwa moja ushawishi usiofaa au zawadi kwa ofisa yeyote wa umma, ndugu zake au watu wenye uhusiano wa kibiashara, kuhusiana na kotesheni hii au baadaye katika utekelezaji wa mkataba kama tutafanikiwa.

Tunayo Sera Dhidi ya Rushwa /Kanuni za Maadili na Programu ya ukubalifu inayojumuisha hatua zote muhimu na za kutosha kuhakikisha kuwa ahadi yetu ya kutotoa rushwa iliyotolewa katika maelezo haya itazingatiwa na menejimenti yetu na waajiriwa na pia watu wengine wote wanaofanya kazi nasi katika miradi ya sekta ya umma au mkataba ikiwa ni pamoja na wakala, washauri, wabia wetu, wakandarasi wasaidizi na watoa huduma wetu. Nakala zetu za Sera Dhidi ya Rushwa /Kanuni za Maadili na Programu ya ukubalifu zimeambatishwa.

FRANCISCO GABRIEL MAPUNDA
*(Jina la mtu aliyepewa mamlaka)*

[signature]
*Sahihi*

23/11/2021
*Tarehe*

______________________
*Muhuri/ Alama ya Kampuni*

55

NTA Level 8 No: 0003409

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# MBEYA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY

*It is hereby certified that*

*Francisco G Mapunda*

*of Registration No: B31341062 has been awarded*

*Bachelor Degree in*

*Civil Engineering*

*After having fulfilled all the requirements for*

Level 8

Upper Second Class

*Issued this 17th day of December in the year 2016*

Deputy Vice Chancellor
(Academic, Research and Consultancy)

Vice Chancellor



UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

# MBEYA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY

BACHELOR DEGREE EXAMINATIONS

## ACADEMIC TRANSCRIPT

SPONSOR : PRIVATE

( Built Environment Engineering Department )   Serial No. : 11204

| Name of the Candidate | Birth Date | Sex | Registration No. | Date of Entry | Programme | UQF Level |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MAPUNDA, FRANCISCO G | 02-10-1983 | M | B31341062 | 2013/2014 | BACHELOR OF ENGINEERING IN CIVIL | 7 - 8 |

| Semester | Module Code | Module Name | Grade | Date Appeared |
|---|---|---|---|---|
| I | CEH 7101 | ENGINEERING SURVEY I | B | 2014 |
| I | CEH 7102 | CONSTRUCTION TECHNOLOGY | B+ | 2014 |
| I | CEH 7103 | FLUID MECHANICS | B | 2014 |
| I | CEH 7104 | CIVIL ENGINEERING MATERIALS I | B | 2014 |
| I | CEH 7105 | MECHANICS OF STRUCTURES | A | 2014 |
| I | CEH 7106 | ENGINEERING GEOLOGY | B+ | 2014 |
| I | CEH 7107 | CONCRETE TECHNOLOGY | C | 2014 |
| I | COH 7102 | COMPUTER PROGRAMMING I | A | 2014 |
| I | GSH 7101 | LINEAR ALGEBRA AND CALCULUS | B+ | 2014 |
| I | GSH7105 | COMMUNICATION SKILLS | B | 2014 |
| II | CEH 7208 | ENGINEERING SURVEY II | A | 2014 |
| II | CEH 7209 | FLUID MECHANICS AND HYDRAULICS | B | 2014 |
| II | CEH 7210 | BUILDING PLANNING AND DRAWING | B+ | 2014 |
| II | CEH 7211 | STRUCTURAL ANALYSIS I | B | 2014 |
| II | CEH 7212 | CIVIL ENGINEERING MATERIALS II | B+ | 2014 |
| II | CEH 7213 | SOIL MECHANICS | B | 2014 |
| II | CEH 7214 | ENGINEERING HYDROLOGY | C | 2014 |
| II | CEH IPT 01 | INDUSTRIAL PRACTICAL TRAINING | A | 2014 |
| II | COH 7202 | COMPUTER PROGRAMMING II | A | 2014 |
| II | GSH 7202 | ADVANCED CALCULUS | C | 2014 |
| III | CEH 7315 | QUANTITY SURVEY | B | 2015 |
| III | CEH 7316 | STRUCTURAL ANALYSIS II | B | 2015 |
| III | CEH 7317 | GEOMETRIC DESIGN AND TRAFFIC ENGINEERING | C | 2015 |
| III | CEH 7318 | REINFORCED CONCRETE DESIGN AND DETAILING I | C | 2015 |
| III | CEH 7319 | FOUNDATION ENGINEERING | B+ | 2015 |
| III | CEH 7320 | HIGHWAY ENGINEERING MATERIALS | B | 2015 |
| III | GSH 7303 | DIFFERENTIAL EQUATIONS | B+ | 2015 |

| Semester | Module Code | Module Name | Grade | Date Appeared |
|---|---|---|---|---|
| IV | CEH 7421 | QUANTITY SURVEYING II | A | 2015 |
| IV | CEH 7422 | REINFORCED CONCRETE DESIGN AND DETAILING-II | B+ | 2015 |
| IV | CEH 7423 | CONSTRUCTION MANAGEMENT | B+ | 2015 |
| IV | CEH 7424 | WATER SUPPLY ENGINEERING | B+ | 2015 |
| IV | CEH 7425 | CONTRACT PLANNING AND ADMINISTRATION | B | 2015 |
| IV | CEH 7426 | PAVEMENT DESIGN AND CONSTRUCTION | B | 2015 |
| IV | CEH 7427 | RESEARCH METHODOLOGY | B+ | 2015 |
| IV | CEH IPT 02 | INDUSTRIAL PRACTICAL TRAINING | A | 2015 |
| IV | GSH 7404 | STATISTICS AND NUMERICAL ANALYSIS | B | 2015 |
| IV | GSH 7406 | ENTREPRENEURSHIP EDUCATION I | B | 2015 |
| I | CEB 8128 | ENGINEERING ECONOMICS | B+ | 2016 |
| I | CEB 8129 | STRUCTURAL STEEL DESIGN | C | 2016 |
| I | CEB 8130 | WASTE WATER MANAGEMENT | A | 2016 |
| I | CEB 8131 | PAVEMENT MAINTENANCE | B+ | 2016 |
| I | CEB 8132 | CONSTRUCTION OF MULTI-STOREY STRUCTURES | B+ | 2016 |
| I | CEB 8134 | IRRIGATION ENGINEERING | B+ | 2016 |
| I | CEB 8136 | BUILDING SERVICES | B+ | 2016 |
| I | CEB P 01 | PROJECT I | A | 2016 |
| II | CEB 8237 | DESIGN OF MASONRY AND RETAINING STRUCTURES | B | 2016 |
| II | CEB 8238 | STRUCTURAL TIMBER DESIGN | B | 2016 |
| II | CEB 8239 | SOLID WASTE MANAGEMENT | A | 2016 |
| II | CEB 8240 | INDUSTRIAL BUILDING CONSTRUCTION | B+ | 2016 |
| II | CEB 8242 | HYDRAULIC STRUCTURES | A | 2016 |
| II | CEB 8243 | WATER RESOURCES MANAGEMENT | B | 2016 |
| II | CEB P 02 | PROJECT II | A | 2016 |
| II | GSB 8201 | ENTREPRENEURSHIP EDUCATION II | B | 2016 |

Cumulative Grade Point Average : 3.7   CLASSIFICATION : UPPER SECOND CLASS

**************************END **************************

Dr. M. I. LINGWANDA
DIRECTOR OF UNDERGRADUATE STUDIES

DATE : January 23, 2017

DIRECTOR OF UNDERGRADUATE STUDIES
MBEYA UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY